



CHUO CHA HERMARGS

Mkuu wa Chuo cha HERMARGS chenye usajili Na. **REG/HAS/205** kilichopo Morogoro (Kinyenze - Kipera karibu na Chuo Kikuu Mzumbe) anayo furaha kuutangazia Umma nafasi za masomo katika ngazi za Astashahada na Stashahada (Certificate and Diploma levels) ya **Ustawi wa Jamii** (Social Work) na **Famasia** (Pharmacy and Pharmaceutical Science) yatakayoanza Oktoba, 2024 kwa **mwaka wa masomo 2024/2025**.

Sifa za Mwombaji kwa Astashahada au Stashahada ya Famasia (Pharmacy and Pharmaceutical Sciences)
Awe amehitimu Kidato cha Nne (Form IV) na kuwa na ufaulu wa kuanzia alama **D** katika masomo angalau manne (4) isipokuwa ya dini ambapo masomo mawili kati ya hayo yawe ni **Kemia na Baiolojia**.

Sifa za Mwombaji kwa Astashahada au Stashahada ya Ustawi wa Jamii (Social Work)
Awe amehitimu Kidato cha Nne (Form IV) na kuwa na ufaulu wa kuanzia alama D katika masomo manne (4) isipokuwa masomo ya DINI. Pia kwa Diploma awe mhitimu wa kidato cha sita (Form VI) na kuwa na ufaulu kuanzia alama E na S katika masomo MAWILI au kuwa na Cheti cha Ustawi wa Jamii au fani nyingine inayoendana.

MUDA WA MASOMO KWA NGAZI ZA ASTASHAHADA NA STASHAHADA

1. Masomo kwa ajili ya Astashahada (Cheti/Certificate) yanasomwa kwa miaka miwili (NTA Level 4 & NTA Level 5) kwa Famasia na Ustawi wa Jamii.
2. Masomo kwa ajili ya Stashahada (Diploma) yanasomwa kwa miaka mitatu (NTA Level 4, NTA Level 5 & NTA Level 6) au kwa Mtu aliye na Cheti atasoma Mwaka mmoja kwa Famasia na miaka miwili kwa Ustawi wa Jamii

FOMU ZA KUJIUNGA

Kwa sasa kuna mfumo wa Udahili wa pamoja yaani **Central Admission System (CAS)** kwa Kada za Afya (Famasia) kupitia tovuti ya NACTVET www.nacte.go.tz kisha utabofya **Maombi ya Udahili Vyo vya Afya** na fuata maelekezo. **Kwa Ustawi wa Jamii (Social Work) maombi yatumwe chuoni.** Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi:-

1. Ofisi ya Chuo kwa simu namba 0742 759 220, 0678 532 890 na 0787 047 650
2. Kwa Barua pepe ifuatayo: hermargs.institute@gmail.com
3. Pia tembelea Tovuti ya Chuo: www.hermargs.ac.tz

MUDA WA KUTUMA MAOMBI

Muda wa kutuma maombi awamu ya kwanza ni kuanzia Tarehe **27 Mei, 2024** mpaka Tarehe **20 September, 2024**

GHARAMA ZA KUTUMA MAOMBI NA NAMNA YA KULIPA

Gharama ya kutuma maombi kwa Ustawi wa Jamii ni **TSh. 30,000/=** yanapatikana pia kwenye fomu au Tovuti ya Chuo (www.hermargs.ac.tz) na Famasia ni **Tshs 15,000** kwa chuo kimoja na **Tshs 30,000** kwa vyo vya zaidi ya kimoja.

NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

Ustawi wa Jamii watume maombi yao Chuoni na kwa **Famasia** watume kwa njia iliyoelekezwa hapo juu, pia unaweza kuwasiliana na Chuo ukasaidiwa kuomba NACTVET. Kwa FAMASIA ukiingia kwenye tovuti ya NACTVET na kubofya **Maombi ya Udahili Vyo vya Afya** na fuata maelekezo ili kuchagua **Chuo cha HERMARGS** kinachopatikana **Morogoro** pamoja na kozi yako pendwa.

GHARAMA ZA MASOMO CHUONI KWA MWAKA NA UTARATIBU WA MALIPO

Ada na michango yote kwa **Famasia** mwaka wa kwanza ni **TSh. 2,435,000/=** na **Ustawi wa Jamii** ada na michango ni **TSh. 1,650,000/=** kwa mwaka. Ada hizi zinaweza lipwa kwa awamu zisizozidi nne.

CHUO KINATOIA HUDUMA YA MALAZI (HOSTELI) BURE KWA WANAFUNZI WOTE

**KARIBUNI SANA
MKUU WA CHUO**